

## HALMASHAURI YA WILAYA YA MKALAMA



OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA,  
S. L. P. 1007  
MKALAMA

Simu Na. 026 2924000

Barua pepe: ded.mkalamadc@singida.go.tz

Tovuti: [www.mkalamadc.go.tz](http://www.mkalamadc.go.tz)

### TAARIFA KWA UMMA NA VYOMBO VYA HABARI

Baada ya kutokuwa na matokeo mazuri katika matokeo ya mtihamu wa darasa la saba uliofanyika mwaka jana, Wilaya ya Mkalama imepewa nafasi ya kuadhimisha juma la Elimu kitaifa ili kuweza kujadili kwa kina na kuzipatia ufumbuzi sababu mbalimbali zilizopelekea kupatikana kwa matokeo hayo.

Maadhimisho hayo yaliyoratibiwa na Mtandao wa Elimu Tanzania (TENMet) kwa kushirikiana na Serikali chini ya Wizara ya Elimu yanatarajia kuanza Mei 14 mwaka huu na yatafunguliwa rasmi na Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe. Daktari Rehema Nchimbi.

Kazi kubwa itakayofanyika katika kipindi chote cha maadhimisho ni kutoa fursa kwa wadau mbalimbali wa Elimu yakiwemo mashirika zaidi ya 180 yanayounda mtandao wa Elimu kuainisha changamoto mbalimbali na kufanya majadiliano ya pamoja na wananchi juu ya jambo la kufanya ili kuweza kupunguza au kumaliza changamoto hizo.

Kwa muda wa Siku nne, tangu kufunguliwa kwa juma hilo, timu yenye wajumbe kutoka Mtandao wa Elimu Tanzania, waandishi wa habari na viongozi mbalimbali wa Wilaya ya Mkalama itatembelea shule sita za Msingi na Sekondari zikiwemo zile zilizofanya vibaya sana katika matokeo ya Mwaka jana ambako itafanyika mijadala mbalimbali kwa kupokea maoni ya wazazi na walezi wa watoto wanaosoma katika shule hizo na kuwafikishia jumbe mbalimbali za Elimu kwa mwaka huu zinazolenga kusisitiza wajibu wa kila upande katika kuhakikisha mwanafunzi anapata Elimu bora.

Mbali na ziara ya timu hiyo, Maadhimisho hayo yanatarajiwa kuambatana na huduma ya utoaji elimu kuhusu mambo muhimu yanayogusa jamii itakayotolewa katika viwanja vya Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama ambapo wataalam mbalimbali watakuwa tayari kujibu maswali kutoka kwa wananchi.

Maadhimisho hayo ambayo kitaifa Mwaka huu yatabebwa na ujumbe usemao “**Uwajibikaji wa pamoja kwa elimu bora kwa wote**” yanatarajiwa kufungwa Mei 18 na Naibu waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) Mhe. Joseph Kakunda.

Omary S. Mtamike  
Afisa Habari (H/W)

**MKALAMA**

09 Mei, 2018.